Kodi ya SIM:

Wananchi wazungumzia hali halisi na kutoa maoni

1. Utangulizi

Mnamo tarehe 25 Juni, 2013, bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 ilipitishwa Bungeni. Bajeti hii ilipitishwa katika kikao cha majadiliano ambapo wabunge 235 walipiga kura wakiikubali na 35 wakiikataa (wabunge 83 hawakuwepo). Mkazo uliwekwa katika kuongeza kodi, kama njia ya kuinua mapato ili kuigharimia bajeti hii iliyofikia TZS trilioni 18.2.

Siku chache baada ya kupitishwa kwa bajeti, ilionekana kuwa Serikali ilikuwa imeanzisha tozo ya kila mwezi ya TZS 1,000 kwa kila kadi ya simu ya mkononi (Sim card). Jambo la kushangaza lilikuwa, wabunge pamoja na wananchi wa kawaida waliokuwa wakifuatilia hotuba ya bajeti walidai kuwa kodi hiyo, iliyojulikana kama "Kodi ya Kadi ya SIM", haikujadiliwa Bungeni. Hili lilizua mjadala wa kitaifa miongoni mwa wabunge wenyewe, makampuni ya simu, vyombo vya habari, wataalamu na wananchi kwa ujumla.

Muhtasari huu unatoa matokeo mapya kuhusiana na mdahalo wa Kodi ya SIM yanatokana na awamu ya tano ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti wa kwanza wa kitaifa barani Afrika unaokusanya takwimu kwa njia ya simu za mkononi. Utafiti ulifanyika kati ya Julai 16 na 30, 2013; na takwimu hizo zinajumuisha majibu kutoka kwenye kaya 1,708. Muhtasari huu pia unawasilisha matokeo kutoka *National Panel Survey, 2010-2011*; na utafiti wa msingi wa *Sauti za Wananchi* ambao ulifanyika kati ya Oktoba na Desemba, 2012. Utafiti wa msingi uliendeshwa katika kaya 2,000 kwa mahojiano ya ana kwa ana.

Muhtasari huu umeandikwa na kuchapishwa na Uwazi iliyo Twaweza, inayopata ufadhili wa Hivos. Umetolewa Septemba 2013

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 Faksi: +255 22 266 4308.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Matokeo makuu ni kwamba:

- Kodi ya SIM ni sawa na gharama za muda wa hewani ya wiki moja kwa kaya ya watu wenye hali duni.
- Zaidi ya nusu ya waTanzania hawafahamu kuhusu Kodi ya SIM
- Watanzania walio wengi (asilimia 83) hawakubaliani na uanzishwaji wa Kodi ya SIM

2. Mambo manne makuu kuhusu Kodi ya SIM

Jambo la 1: Asilimia 80 ya kaya zinamiliki walau simu moja ya mkononi

Takwimu za utafiti wa *Sauti za Wananchi* zinaonyesha kuwa umiliki wa simu za mkononi nchini Tanzania ni wa kiwango cha juu zaidi mijini. Hata hivyo, wananchi walio wengi katika kaya za vijijini (asilimia 75) wanaishi katika kaya ambayo walau mwanakaya mmoja anamiliki simu ya mkononi. Kielelezo cha 1 hapo chini kinaonyesha kuwa kaya tajiri zaidi[1] zina uwezo walau wa mara mbili zaidi, wa kumiliki simu ya mkononi ukilinganisha na kaya zawatu wenye hali duni. Hata hivyo, moja kati ya kaya mbili maskini zinamiliki simu ya mkononi. Hii ina maana kwamba mabadiliko yanayogusa gharama za mawasiliano ya simu za mkononi yanamgusa karibia kila mtu bila kujali ni wa kipato gani.

Kielelezo cha 1: Umiliki wa simu za mkononi katika ngazi za kaya miongoni mwa kundi ya mapato



Chanzo cha data: Sauti za Wananchi, Utafiti wa Msingi, Oktoba – Desemba, 2012

[1] Wahojiwa matajiri na maskini zaidi wanatofautishwa kwa kutumia faharisi ya utajiri ambayo inakokotolewa kwa kutumia umiliki kwa kaya wa amana zilizochaguliwa, ambapo asilimia 20 ya wahojiwa wako katika kundi la maskini zaidi.

Jambo la 2: Kodi ya SIM ni sawa na gharama za muda wa hewani ya wiki moja kwa watu wenye hali duni

Je, watanzania wanatumia kiasi gani kununua muda wa hewani? Takwimu zilizoonyeshwa hapo chini zinatokana na Utafiti wa *National Panel Survey 2010-2011*[2] (NPS, kwa upande wa Bara pekee). Kielelezo cha 2 kinaonyesha mgawanyiko kwa wastani wa gharama za muda wa hewani kwa kutazama makundi ya mapato.



Chanzo cha data: NBS*, National Panel Survey*, 2010-2011.

NPS ilihoji maswali mbalimbali kuhusu matumizi ya kaya. Kwa vocha za simu, takwimu zilionyesha kuwa asilimia 56 ya watanzania walinunua muda wa maongezi siku 30 kabla ya mahojiano hayo na, kwa wastani, walitumia TZS 16,348.

Kwa kuwa Kodi ya SIM ina thamani isiyobadilika, watu wenye hali duni huathirika vibaya zaidi. Asilimia 10 ya watu waliopo katika kaya zenye hali duni zaidi wanatumia chini ya TZS 1,000 ya Kodi ya SIM kwa wiki kununua muda wa hewani.

Jambo la 3: Zaidi ya nusu ya watanzania hawafahamu kuhusu kodi ya SIM

Kielelezo cha 3: Je, unafahamu kwamba Serikali imeanzisha kodi mpya ya TZS 1,000 ya Chipu ya simu?

[2] Ofisi ya Takwimu ya Taifa -- National Bureau of Statistics (NBS) [Tanzania]. 2011. Tanzania National Panel Survey Report (NPS) - Wave 2, 2010 - 2011. Dar es Salaam, Tanzania: NBS. (www.nbs.go.tz)



Chanzo cha data: *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi – Awamu ya 5, Julai 2013.

Jambo la 4: Watanzania wengi (83%) hawakubaliani na Kodi ya SIM

Katika makundi yote ya kipato, watu walio wengi, asilimia 83 kwa wastani, hawakubaliani na Kodi ya SIM. Miongoni mwa kaya za watu wenye hali duni zaidi, kiwango pungufu kidogo (71%) ndiyo wasiokubaliana na kodi ya SIM.

Kielelezo cha 4: Je, kwa kiasi gani unakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuanzisha Kodi ya SIM?



Chanzo cha data: *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi – Awamu ya 5, Julai 2013.

3. Majadiliano na Hitimisho

Hotuba ya bajeti ya 2013-14[3] ilionyesha kuwa Tanzania ina nakisi ya kibajeti (upungufu) ya kiasi cha TZS trilioni 6.7, ambayo ni sawa na TZS 136,735 kwa kila Mtanzania. Nakisi hiyo hujaziwa na walipa kodi, misaada kutoka kwa wahisani na mikopo itakayolipwa na vizazi vijavyo. Kwa kulinganisha na usuli wa takwimu hizi za bajeti, Kodi ya SIM inaibua maswali matatu. (1) Je, Tanzania ilenge kuwa na bajeti yenye uwiano zaidi? (2) Kama jibu ni ndiyo, je, jambo gani ni bora zaidi, kupunguza matumizi au kuongeza kodi? (3) Kama kuongeza mapato kwa njia ya kodi ni bora, je, Kodi ya SIM ndiyo njia bora zaidi kuliko, mathalani, kodi kwenye mafuta ya petroli?

Majibu rasmi kwa maswali ya (1) na (2) ni, kwa mpangilio huo huo, kiasi fulani chanya na hasi. Ikumbukwe kuwa Bajeti inazingatia vipaumbele vinavyowekwa kwenye mpango wa maendeleo wa mwaka kwa 2013/2014 na jitihada ya *Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now)*[4]. Ili kufikia malengo haya, uwekezaji lazima uendelezwe katika maeneo ya kipaumbele – nishati, usafirishaji, kilimo, maji, elimu, na uhamasishaji rasilimali –: yaani, kutakuwa na matumizi zaidi kuliko kupunguza matumizi ya serikali. Wizara ya Fedha imepewa jukumu la kutafuta rasilimali hizi ili kugharimia matumizi wakati ikifanya jitihada ya kudhibiti ukopaji. Kama mwongozo wa bajeti unavyoeleza: “Kwa kuzingatia upana wa makusanyo ya mapato, Serikali itaimarisha udhibiti na utawala wakodi na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani” (Mwongozo, Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, 2012; p36).[5]

Katika muktadha huu, je, Kodi ya SIM ni zana bora ya kodi? Uchambuzi wa kiuchumi na nadharia ya kodi zinaeleza kanuni nzuri lakini ambazo zinakinzana: (a) kodi zinapaswa kuwa rahisi kuzikusanya na kuzisimamia kwa gharama ndogo(b) kodi zinapaswa kutobadili maamuzi ya kiuchumi kwa kiasi kidogo kadiri inavyowezekana (c) jamii inapaswa kuona kuwa baada ya kukusanya kodi mgawanyo wa mapato ni wa “haki”.

Kodi ya SIM inayo matokeo mazuri kulingana na maswali mawili ya mwanzo: makampuni ya simu yana usimamizi thabiti wa wateja ambao unafanya usimamizi wa kodi uwe rahisi wakati ambapo kodi hiyo ni kwa mara moja” – haihusiani ni na kiasi mteja anachotumua kupiga simu. Kwa wachumi, hiki ndicho kile

[3] Kwa Kiswahili: http://www.mof.go.tz/mofdocs/msemaji/HOTUBA%20YA%20SERIKALI-BAJETI.pdf; kwa Kiingereza: http://www.mof.go.tz/mofdocs/msemaji/Budget%20english%202013.pdf.

[4] *Matokeo Makubwa Sasa* inalenga kuchochea mabadiliko katika sekta sita za msingi: nishati na gesi asilia, kilimo, maji, elimu, usafirishaji, na uhamasishaji rasilimali. http://www.pmoralg.go.tz/quick-menu/brn/index.php

[5] Chanzo cha data: Miongozo ya maandalizi ya mpango wa mwaka na bajeti ya 2012/13, muundo wa bajeti ya Tanzania, Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, 2012.

kinachotafutwa sana lakini ni vigumu kukipata: kwani, unapokuwa umeshalipa kodi ya TZS 1,000, tozo ya matumizi yako ya simu na jinsi unavyoitumia haya ni mambo ambayo hayaathiriwi tena na kodi. Lakini hoja hii ya kiufanisi wa makusanyo ndiyo pia udhaifu wake: kwa kuwa kodi hii haibadiliki kulingana na kipato cha mtu, “wanaoumia zaidi ni watu wa kipato cha chini”. Hii ina maana kwamba Kodi ya SIM ni ya kiwango cha juu zaidi kwa upande wa watu walio maskini zaidi. Je, hii kodi ya aina hii ni ya haki?

Hata hivyo, jambo la manufaa zaidi kwa Wizara ya Fedha ni kwamba Kodi ya SIM inawakilisha lengo linalopigiwa kelele sana, nalo ni la: kupanua wigo wa kukusanya kodi. Hii ni njia inayosambaza kodi kwa idadi kubwa ya watu wanaotumia simu, ambayo inakua kwa kasi; kwamba watu wengi zaidi wanachangia kwenye mapato ya taifa. Kupanua wigo wa kodi ni jambo linalokubalika kiuchumi (wachangiaji zaidi wanapunguza upindishaji wa mzigo wa kodi za ndani) na kisiasa (utozaji kodi unahitaji uwakilishi, unajumuisha) lakini kinachohitajika ni manufaa ya matumizi ya umma yanayotokana na makusanyo hayo, kuwa matokeo yawe yale yanayopimika, na yanayoonekana, na yaliyoenezwa nchi nzima. Hakuna kutoza kodi pasipo na uwajibikaji.

Hata hivyo, hoja kubwa ya wanaopinga kutoza kodi Kadi za SIM ni uwezo wake mkubwa wa kukuza uchumi. Utafiti wa hivi karibuni (Aker and Mbiti, 2010) unaonyesha njia nne ambazo simu za mkononi zinavyonufaisha uchumi wa nchi za Afrika. Kwanza, simu za mkononi zinakuza upatikanaji na matumizi ya taarifa: hii inapunguza gharama za utafiti na kuongeza ushindani na ufanisi wa masoko na makampuni. Pili, simu za mkononi ni sekta ya ukuaji, zinatengeneza nafasi za kazi lakini pia mwendelezo wa mmiminiko wa teknolojia mpya. Tatu, simu za mkononi zina uwezekano wa kuimarisha mifumo isiyo rasmi ya bima, kwa kupeleka ujumbe baina ya wanafamilia hata kama wanaishi mbalimbali sana. Nne, simu za mkononi zina fursa ya kuongeza utoaji huduma, katika afya, elimu na kilimo, lakini hasa katika masuala ya fedha: kadi za SIM zinazidi kutumiwa kwa kutuma na kupokea fedha na hata huduma za kibenki hasa vijijini ambako hakujaunganishwa na mifumo ya kibenki. Mtiririko wa taarifa na huduma za fedha ni mambo muhimu kwa ukuaji wa uchumi, na kinachowagusa wengi ni kwamba Kodi ya SIM isije ikaharibu au kurudisha nyuma utaratibu huo.

Muhtasari huu umetoa takwimu muhimu kuhusu Kodi ya SIM kwa kulinganisha matumizi ya watu na vipato, maoni ya watu kuhusu jambo hilo, na mjadala mfupi kuhusu kufaa kwake kama zana ya utozaji kodi na usimamizi wa bajeti. Tunachosisitiza ni kwamba uchambuzi makini na mjadala wa masuala haya unapaswa kuimarisha uelewa wetu kuhusu kama Kodi ya SIM ibaki kama ilivyo au ifutwe.